# MZEE RUKHSA: SAFARI YA MAISHA YANGU

**ALI HASSAN MWINYI**

**SIMULIZI YA – PROFESA RWEKAZA SYMPHO MUKANDALA**

## 1. UTANGULIZI

Ilikuwa siku ya Ijumaa, tarehe 8 Mei, 1925 alizaliwa mtoto wa kiume pekee kati ya watoto watano Magondi na Bi. Asha Mwinyi-Shehe wa Mzee Hassan Mwinyi katika kijiji cha Kivure, Wilaya ya Mkuranga, Mkoa wa Pwani. Kijiji hiki kilikuwa kando ya Barabara kuu itokayo Dar es Salaam hadi Kisiju pwani.

Kitabu hiki ni simulizi ya safari ya maisha ya kijana huyu tangu siku ile mpaka leo hii. Ni kitabu chenye kurasa mia nne tisini na moja (491), zilizogawanywa kwenye sura thelathini na moja, pamoja na viambatanisho na picha nyingi nzuri. Utangulizi wake umeandikwa na Mh. Benjamin Mkapa, Rais wa tatu wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania. Simulizi hii imefanywa kwa ufasaha na ustadi wa hali ya juu sana, kwa Kiswahili murua. Pale ambako mwandishi anaona msamiati wake ni mkali, basi anasaidida kwa tafsiri yake mwenyewe aidha kwa Kiswahili ama kiingereza. Kitabu hiki kina maneno ……….. ambayo yamehaririwa na kuchapwa kwa umakini mkubwa na mchapishaji wa kitabu hiki Mkuki na Nyota. Sikubaini kosa hata moja.

Katika kitabu hiki, Mzee Rukhsa anajaribu kuyapa majibu baadhi ya maswali mengi ambayo yamekuwa yakimfuata kila alipokwenda. Kwa mfano,

- Je asili yake ni nini? Ni mbara au muunguja? Kama ni mbara ilikuwaje akaishia unguja?
- Kwa nini alijiuzuru uwaziri hapo mwaka 1974. Ilikuwa kwa hiari au alishinkizwa na mwalimu?

- Ilikuwaje akamrithi Alhaji jumbe mwaka 1984, wakati kulikuwa na Wazanzibari wengine labda mashuhuri zaidi, na waliotaka huo urausi.
- Ilikuwaje akamrithi mwalimu hata kama haikuwa chaguo lake la kwanza?

Wasilisho hili linamega simulizi hii katika sehemu kuu nne. Sehemu ya kwanza ni mwanzo wa safari hii huko Kivure, wakati wa machweo ya jua, kukiwa kunapambazuka ardhi imejaa umande, ndege wakifurahia mwanzo wa siku mpya. Hapa tunaelezwa kuzaliwa kwake, malezi, na elimu. Sehemu ya pili, ni nyakati za mchana, adhuhuri na Bwana msafiri sasa mtu mzima anaanza kazi serikalini mpaka kuwa waziri. Katika sehemu ya tatu, Saa za alasiri, mambo yanakolea, Mh. Ali Hassan Mwinyi ana kuwa Raisi wa kwanza wa Zanzibar na baadae wa Muungano. Hatimaye baada ya kazi nzito yanafika mawio ya jua, majira ya jioni na msafiri wetu anashuka milimani kwa mapumziko stahiki.

## 2. KUZALIWA MALEZI NA ELIMU

Safari ya maisha ya kijana huyu ilianzia hapo kivule, alipozaliwa alipewa jina la **Sihaba.** Kusudio lake likiwa kumshukuru Mungu kwa wazazi wake kupata mtoto wa kiume. Baada ya mda mfupi, wazazi waliamua kumuita **Nzasa.** Tunaelezwa kuwa Nzasa ni sehemu ya ardhi inayokuwa majimaji au chepechepe, daima haikauki milele. Baba wa kijana ndiye aliyepwa jina hili kwanza hapo kijijini, kwani alikuwa haishiwi hata siku moja. Akiitwa mzee Nzasa, aliitikia "hainywei" yani halikauki. Hatimaye mzee akaamua kumuita mwanae pia Nzasa, kama Baraka ili naye katika uhai wake asije kaukiwa. Mzee Rukhsa anasema hadi leo anaona Mwenyezi Mungu

alikubali dua hiyo ya Baba yake. Anasema “sijawahi kukopa katika maisha yangu yote”

Safari ya kusaka elimu ilianzia alipokuwa na miaka minne, alipoondoka kijijini Kivule, akapelekwa na Baba yake hadi Zanzibar kwa rafiki mkubwa wa Baba yake Mzee Suwedi Bin Mgeni. Hapa alianza kujenga msingi wa maisha yake kwa kwenda shule kusomea Quran, akitarajia baadae kusomea ushekhe. Baada ya chuo cha Quran Mangapwani, alijiunga na shule ya Msingi Mangapwani (1933) akiwa na umri wa miaka nane na nusu.

Nyumbani kwa Mzee Suwedi bin Mgeni, Kijana Ali ilibidi kila siku kabla hajaenda shule kukusanya vyungu na sufuria vilivyopikiwa kwenda kuviosha. Kwa kuwa vilikuwa vikubwa sana kwa kimo chake ilimlazimu kuvikumbatia toka jikoni hadi nje mwisho wa uwanja. Hivyo alijieneza masizi ya vyungu hivyo nguoni na mwilini. Anasema alipokwenda shuleni baadae alikuwa mchafu kuliko yule kisonoko wa hadithi.

January 1937 kijana Ali alikuwa mmoja wa wanafunzi wawili kutoka darasani kwake waliochaguliwa kwenda darasa la tano shule ya kati Dole. Hapo kwa mara ya kwanza alishuhudia ubaguzi wa rangi kwani wanafunzi wa kiarabu waliishi bweni lao pekee.

Kati ya mwaka 1943 mpaka1944 alisomea Ualimu Dole kwani hiyo ilionekana kuwa elimu ya juu kabisa wakati ule. Baadae alihamishiwa Bumbwini ambapo ilibidi asimamie ujenzi wa shule atafute wanafunzi na kuwafundisha vizuri.

Safari ya kujenga msingi wa maisha iliendelea hapo mwaka 1954, Aprili, Mwalimu Ali alipata fursa ya kwenda kusomea ualimu nchini Uingereza

katika chuo kikuu cha Durhan mpaka 1956. Katika mwaka wa masomo 1961/62 alipelekwa tena na serikali kushikizwa kwenye Chuo Kikuu cha Hull, Leicester, Uingereza. Mwaka 1962, akarudi Zanzibar na kuteuliwa kuwa mkuu wa Chuo cha Ualimu na huu ndo ulikuwa mwisho wa majira ya asubuhi ya safari hii ndefu.

## 3. MAISHA NA KAZI

Ikiwa ni adhuhuri sasa, katika safari yake ndefu ya maisha, Bwana Ali alianza maisha ya kazi na utumishi katika serikali. Upepo wa mapinduzi haukumwacha nyuma. Bwana Ali. Aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu Wizara ya Elimu mwaka 1964.

Anasema:

"Wengi wetu tulikuwa hatuna uzoefu na kazi tulizopewa. Tukaambiwa tujifunze humohumo. Tukachechemea lakini upepo wa ari na matumaini ukajaa katika taifa. Jahazi la utumishi wa serikali likasafiri" Pg. 87. Mda kidogo baadae aliteuliwa kuwa naibu Mkurugenzi Mkuu wa Chama Muhimu cha Walima Karafuu kilipo taifishwa.

Mwaka 1970 alipata simu anaitwa Ikulu Zanzibar, na gari la polisi likamfuata ila alikataa kulipanda akisema "kwa kuwa mie sio mfungwa, wala mtuhumiwa nitakwenda mwenyewe." Walifukuzana na Polisi hadi Ikulu huku gari ya polisi wakiwasha taa na kupiga honi. Fikra za kila aina zilimjia kwani hakujua anaitiwa nini, na kama atakuwa salama. Hapo Ikulu alijipa mda kidogo atulie, kujifuta jasho usoni na miguuni, na kukusanya pumzi. Hatimaye akaenda na kumsalimu Mh. Rais Karume. Rais Karume akamwambia Rais Nyerere ameomba majina mawili ili amteue mmoja Waziri.

Akamwambia jina lake lilikuwa moja wapo. Akamshauri asikilize taarifa ya habari saa mbili usiku.

Mh. Ali Anasema:

"Moyo wangu ulijaa mchanganyiko wa uoga na furaha isiyoelezeka, tamaa yakupata, na hofu ya kukosa" Pg. 88.

Usiku ule akawa ameteuliwa kuwa Waziri wa Nchi (Ofisi ya Rais).

Anasema:

"Nililala Mwalimu nikaamka waziri katika Serikali ya Muungano".

Wakati wa kuapa ilikuwa mara yake ya kwanza kukutana na Mwalimu J.K. Nyerere.

Ila anasema kwa mwaka wote 1971 alikuwa waziri lakini asiyekuwa na shughuli iliyotamkwa. Katibu Mkuu Kiongozi Mzee Dickson Nkembo naye hakunipa jibu la sawa sawa anasema. Mwaka 1972 aliteuliwa kuwa Waziri wa Afya hadi mwaka 1975. Mwaka huo hakushiriki katika uchaguzi mkuu lakini Mwalimu Nyerere alimteua kuwa Mbunge na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Miaka miwili baadae 1977 ilibidi kujiuzulu baada ya mauaji huko Mikoa ya Mwanza na Shinyanga. Anasema alijiuzuru mwenyewe bila shinikizo kutoka kwa Mwalimu au mtu mwingine. Katika sentensi ya mwisho ya barua ile, alisema "kwa fedheha, hili, naomba unikubalie nijiuzulu. Barua kamili ya kujiuzulu imeambatanishwa katika kitabu hiki.

Mh. Ali anasema kinacho sikitisha ni kuwa mauaji kama hayo yanaendelea zaidi ya miaka arobaini baadae. Baada ya kutumika kama Balozi huko Misri tangu 1978, Octoba 1981 aliteuliwa tena kuwa Waziri wa Mali Asili

na Utalii, na hatimaye akateuliwa tena Waziri wa Nchi alipoanzia Ofisi ya Rais (Muungano).

Wakati huo alikuwa anaishi nyumba ya serikali Osterbay. Basi wakati anajenga nyumba yake hapo Mikocheni. Alikuwa anaweka vifaa vyake vya ujenzi hapo nyumbani Osterbay basi baada ya mabadiliko ya Mawaziri, nyumba ya Osterbay akapangiwa Waziri mwingine. Mh. Ali anasema waziri mpya alikuja nyumbani nakunitaka nimpishe mara moja niende kwetu Zanzibar. Sikutaka ugomvi, nikajiondokea na kumuachia nyumba pamoja na vifaa vyangu vya ujenzi akavichukua. Nami sikumdai. Nilipokuwa alikuwa na wasiwasi ila Rais nikaendelea kumpa Uwaziri.

## 4. URAIS WA ZANZIBAR NA WA MUUNGANO

Kuna mambo mawili kuhusu urais wa Zanzibar. Kwanza hakuutegemea. Mh. Ali Hassan alialikwa kikao cha CCM Dodoma Januari 1982. Alikuwa waziri na mjumbe wa NEC, hakuwa mjumbe wa kamati kuu. Alikosa malazi stahiki nakuishia kwenda kukaa kwenye chumba cha wanafunzi Chuo cha Biashara (CBE) Dodoma. Kikao chenyewe anasema kilikuwa kigumu sana. Kilipangiwa siku tano lakini kikachukua siku 7. Anasimulia kuwa kulikuwa na makundi mawili kutoka Zanzibar ambayo yalihasimiana sana. Kundi la kwanza lilijulikana kama **Wakombozi** na walinzi wa mapinduzi. Kundi la pili walijiita **Frontliners** wakuleta mabadiliko. Anasema wengine hatukuwa na kundi. Kundi letu lilikuwa Zanzibar. Front Liners ndiyo walioongoza mashambulizi juu ya Rais Jumbe. Hatimaye akajiuzulu tarehe 29, January. Kitendawili kikawa nani atachukua na kukaimu nafasi yake. Wakati hayo makundi mawili yanajipanga, Mwalimu

Nyerere alikuwa na mawazo mengine. Mwalimu siku zote aliheshimu sana mawazo ya Sheikh Thabit Kombo na mara zote alipenda kumsikiliza. Sheikh Thabit Kombo ambaye alikuwa KCMC kwa matibabu. Akatumiwa ndege aje Dodoma. Alipoulizwa kwenye kikao Sheikh Thabit, hakufikiri mara mbili, akasema Ali Hassan Mwinyi.

Mh. Ali anasema aliduwaa kwa jinsi uteuzi wake ulivyopokelewa kwa furaha. Anabaini pia baadae alikuja kufahamu kuwa wazo la kumtafuta Rais mpya asiye na makundi na anayeweza kuwaunganisha Wazanzibari lilianza mapema zaidi, tangu akiwa Balozi Misri Jina lake lilizunguka mara kwa mara katika mazungumzo hayo.

Wakati anakaimu, NEC ilikaa March 10, 1984, kujadili wagombea wa Rais katika uchaguzi maalum wa kumchagua Rais wa Zanzibar. Yalipendekezwa majina mawili na wote walikuwa hawakuomba. Sheikh Idrissa Abdulwakil aliomba kutoa jina lake kabla ya kupiga kura. Likabaki jina la Mh. Ali Hassan Mwinyi. Sihaba akawa Nzasa

Jambo la pili ni kwamba Dhana ya RUKHSA ilianzia hapa. Mh. Rais Ali Hassan na wenzie walipandisha mishahara ya wafanyakazi, wakalegeza masharti ya wananchi kutembea wanavyotaka, wakazuia watu kukamatwa na kuwekwa ndani hovyo, wakaruhusu sekta binafsi kuingiza chakula nchini, na kuruhusu usafiri wa pick-up kubeba abiria, maarufu kama "chai maharage."

## URAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Mengi yamesemwa kuhusu uteuzi wa Mh. Ali Hassan kuwa mgombea wa kiti cha Urais wa Tanzania. Mh. Ali anabainisha kuwa uteuzi huo ulipitia hatua tatu muhimu.

Kwanza kulikuwa na suala la Mwalimu kung'atuka na kutogombea tena. Tume mbili ziliundwa moja serikalini na nyingine ndani ya chama kuchunguza na kushauri juu ya jambo hili, kwani wapo wengi waliotaka Mwalimu aendelee. Kamati zote zilikubaliana na mawazo ya Mwalimu kuwa ang'atuke, na Mwalimu alifurahi sana.

Pili ikawa swali gumu la nani achukue nafasi yake. Mwalimu aliendesha mchakato huu kwa umakini na demokrasia. Kwanza Mwalimu aliwaongoza wajumbe wa Kamati kuu kubainisha sifa za mgombea anayetakiwa. Baada ya kukubaliana, hatua ya pili ilikuwa Mwalimu kama Mwenyekiti apendekeze majina matatu, na alifanya hivyo. Usiku wa kuamkia siku ya mkutano maalum tarehe 15 August 1985, mwalimu aliwaita chemba wazee kutoka Zanzibar kupata maoni yao. Rais Mwinyi anasema mkutano huo haukuwa mzuri. Karibu wajumbe wote walimtuhumu mgombea mmoja bila ushahidi wala udhibitisho mambo mengi kuwa ni Hizbu, msaliti, na hasemi kauli ya "mapinduzi daima". Katika mkutano kesho yake, mzee kawawa aliomba asijadiane akakubaliwa. Ikawa zamu ya Rais Mwinyi kujadiliwa kwani alikuwa mwendamizi kama Rais wa Zanzibar kwa wawili waliobaki. wajumbe karibu wote walimwagia sifa Mh. Ali. Hassan. Kisha mwalimu akaaamua kuwa "kama hivyo ndivyo basi hakuna haja ya kumjadili mwingine." Hatua ya tatu ilikuwa kwenda kwa wapiga kura. Katika uchaguzi mkuu wa mwaka 1985 Mh. Ali Hassan alichaguliwa kuwa Rais wa awamu ya pili kwa kura nyingi.

Mh. Ali anasema:

> “Mmojawapo aliyejawa na furaha hadi kutokwa machozi alikuwa Mwalimu Nyerere akionesha wazi furaha ya kuhitimisha uongozi wake………

Mara alipotinga Ikulu, jambo la kwanza anasema “Nikatangaza uteuzi wa kijana hodari kuwa Waziri Mkuu na Makamu wa kwanza Rais” Huyu ni Joseph Sinde Warioba. Hii ilitokana na fikra nyingi na pia mashauriano na Mwalimu juu ya jambo hili. Anasema pia jambo lililomsumbua kidogo ni kumhusu Dr. Salim Ahmed Salim ambaye alikuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais, Serikali iliyopita. Baada ya kushauriana na Mwalimu, aliamua kuunda nafasi mpya ya Naibu Waziri Mkuu ili impe heshima anayostahili na kumteua pia kuwa waziri wa ulinzi.

Wakati Rais Mwinyi anakabidhiwa kasia za kuiongoza ngalawa na kuivusha madhoruba makali, kulikuwa na mikondo miwili inaisakama ngalawa hii. Wa kwanza ulikuwa wa uchumi, wa pili wa kisiasa. Ngalawa ilibeba pia watazamaji makini, wakiongozwa na Baba wa Taifa aliyekuwa bado mwenyekiti wa CCM, Mwalimu J. K. Nyerere.

Mikondo yote miwili ililazimu mageuzi ya uchumi, na baadae ya siasa pia. Rais Mwinyi anatueleza kuwa kazi ya mageuzi ya uchumi haikuwa nyepesi kabisa. Ila mageuzi ya uchumi yalikuwa lazima. Mkondo wa uchumi ulikuwa umechafuka kwa zaidi ya miaka kumi. Sera za utekelezaji wa siasa za nchi hususan operasheni maduka, operasheni vijiji, mfumo wa mashirika ya umma yaliyokuwa yanachechemea kwa kujiendesha kwa hasara na kuhitaji ruzuku kubwa, sheria za nguvu kazi, vyote vilichangia kupunguza

uzalishaji: Pia bei duni za mazao, uhaba mkubwa wa bidhaa za kila aina, uhaba mkubwa wa mafuta na chakula, na hatimaye ulanguzi na rushwa. Sheria zilipitishwa March 25, 1983 kuwakamata wahujumu uchumi. Rais Mwinyi anabainisha kuwa kulikuwa na uchumi wa aina mbili-Sambamba – uchumi rasmi wa serikali usio na fedha, na uchumi wa ulanguzi na magendo wenye fedha ambayo ililea rushwa. Mchango hasi katika hali hii pia ulitokana na Benki ya dunia, Fuko la Fedha la Kimataifa, na mataifa kadhaa ya Magharibi yaliyoshinikiza kutimiza masharti ambayo Mwalimu aliyaona kama ni ya Kisiasa.

Rais Mwinyi anabainisha kuwa mazungumzo hayo hakuyaanzisha yeye. Yalianzishwa na Mwalimu ambaye alipambana nao sana kwani walitoa majibu mepesi ya vitabuni na nadharia (P. 205). Hatimaye Mwalimu alilegeza msimamo kidogo. Rais Mwinyi anasema, "Si wengi wa kizazi cha sasa wanaojua kuwa ni Mwalimu Nyerere aliyekubali, japo kwa shingo upande kuwataka wazazi na walezi wachangie gharama za elimu" (cost sharing. P. 209). Mara baada ya kunikabidhi uongozi Mwalimu aliitisha kikao cha kamati Zanzibar. Katika kikao kila akasema: kwa kuwa yeye kang'atuka, basi tuendelee na mazungumzo na wahisani tuitikie makubaliano kwani hali ilikuwa mbaya sana.

Baada ya hapo yalifuata mageuzi kwa kulegeza masharti ya biashara na uwekezaji. N.k.

Mkondo wa pili, mageuzi ya kisiasa nao ulikuwa mgumu sana. Kwanza kabisa Baba wa Taifa alikuwa aachie ngazi ya uenyekiti wa CCM October 1987. Lakini kadri siku zilivyo karibia, yalizuka mashaka na minong'ono.

Wapo wanaosema "waliojiona ndio wahimili wa ujamaa "ambao waliona hawezi  Rais Mwinyi kuaminiwa kulinda ujamaa kwani aliushabikia mno ubepari. Wapo wengine waliodhani kuondoka kwa Mwalimu itakuwa fursa kwao kuchukua madaraka kwani Rais Mwinyi hasingeweza kuwadhibiti na anasema walianza kujipanga. Ili kukata mzizi wa fitna Rais Mwinyi mwenyewe ndiye alipendekeza hapo Octoba, 1987 Mwalimu aendelee kama Mwenyekiti na Mwalimu akakubali.

Lakini juhudi za hao wafaidhina hazikuishia hapo. Kwenye mkutano huo wa kizota, iliwasilishwa Program ya miaka 15 ya chama ambayo haikuzingatia hata kidogo mageuzi ambayo tulikusudia kuyafanya. Hii ilijenga taswira ya kuwa chama na serikali tulikuwa na sera na mwelekeo tofauti. Kwenye mkutano huo huo, msaidizi wangu wa karibu waziri wa fedha Uchumi na mipango, hakuchaguliwa kuingia kwenye kamati kuu ya ccm. Rais Mwinyi anasema "kwa hili wanafidhina wa ujamaa walinifunga goli. Lakini hatimaye hawakushinda mchezo."

Pili lilizuka swala ya kubadili mfumo kuingia kwenye mfumo wa ushindani wa vyama vingi. Kwa ujumla viongozi wote pamoja na Mwalimu tuliridhika na kufurahishwa na mchakato wa mapendekezo. Tulishindana na mwalimu kwenye jambo moja tu la wagombea binafsi. Yeye alitaka wawepo lakini wengi kwenye chama na serikali walihofu kwa haki kabisa kuwa hiyo itakuja kudhoofisha CCM. Pale wasiopita kwenye mchujo wakiamua kusimama kama wagombea binafsi. Pia anasema, "tulijitahidi kufanya iwe vigumu kwa vyama kuungana. Wakasema wakitaka kuungana, lazima wajifute kwanza, kisha kuanza nakujisajili upya.

## Changamoto za Urais

Rais Mwinyi anabaini changamoto kadhaa wakati wa utawala wake.

Kwanza ni swala la maadili ya uongozi. Swala hili liliibuliwa na mwalimu akiwa bado mwenyekiti. Mwalimu alimuomba Comrade Ngombale aandae mada kuhusu hili na alipoiwasilisha alishambuliwa sana. Lakini Rais Mwinyi anasema Comrade Ngombale alikuwa amejiandaa vizuri na aliwagonga sana waliopinga mabadiliko. Alisisitiza kuwa mali si haramu, kilicho haramu ni jinsi mali ilivyotumika. Hatimaye wajumbe wakakubali hoja ya mabadiliko na kingunge akaombwa akaifanyie kazi hoja ya mabadiliko na kuiwasilisha tena NEC. Mwalimu alistaafu AGOSTI, 1990 uenyekiti wa CCM. Hivyo mada ilipowasilishwa tena anasema Rais Mwinyi, "zigo lile lilinikuta mimi ndiye mwenyekiti."

Mabadiliko ya Zanzibar yalipokelewa kwa furaha na wajumbe wengi. Ananukuu Mzee Rashid Kawawa aliyesema " na sisi tuwe Watu " kwani viongozi wa ccm waadilifu waliojiona kama wako jela. Rais mwinyi anakiri kuwa Mwalimu Nyerere baadae alisikika akilaumu maamuzi ya Zanzibar, lakini anasema "Naamini kabisa kuwa kimsingi aliunga mkono dhana ya mabadiliko na wala hakupinga waziwazi utekelezaji wake, ila pengine aliona tumekwenda mbali kuliko alivyokuwa ametarajia."

Swala la pili ni Muungano. Tume ya Nyalali ilikuwa imeibua hoja kuwa tukiingia kwenye mfumo wa vyama vingi basi tuwe na serikali ya shirikisho yenye serikali tatu. Hoja hii ilikataliwa, ila baaadae ikaunganishwa na hoja ya kumpata Mgombea mwenza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano iliyofanyiwa kazi na jaji Bomani. Mara misuguano hiyo ikazaa kikundi cha

G55 kilichotaka Serikali ya Tanganyika. Hii ilijidhihirisha katika kikao cha Bunge cha bajeti cha mwaka 1992/93 hapo August 24, 1993. Rais Mwinyi anasema "yaliyotokea Bungeni yaliniweka mahali pagumu sana. Sitasahau , " Wabunge walipopitisha Azimio kwa kauli moja kuhusu Serikali ya Tanganyika ndani ya muungano , Rais Mwinyi anasema , " katika kile ninachokiona sasa kama ulevi wa hisia kuwa wanaweza kumpuuza Mwalimu na lolote lisitokee."

Anaendelea kuwa "wengine, hasa waliofikiri wameshampiga Mwalimu Nyerere bao la kisigino." Na walitaka tuamini kuwa maji yameshamwagika. Lakini Mwalimu hakukubali alijenga hoja tena na tena na kulaani kitendo kile. Na hatimaye Mwalimu alifanikiwa. Hatimaye katika kikao chake 29 Julai 1994 – 1 August, 1994, NEC ilitoa Azimio lililoweka wazi msimamo wa CCM na tulimaliza jambo hili. Rais Mwinyi anasema "katika mambo nayajutia katika uongozi wangu ni kuliachia jambo hili likatokota hadi kufikia azimio hilo la Bunge."

Katika kitabu chake **Uongozi wetu na hatima ya Tanzania** Mwalimu "alinikosoa mimi binafsi, na simlaumu"(300)

Jambo lingine lililomuudhi sana Mwalimu ni kile alichokiita woga wa viongozi. Rais Mwinyi ananukuu Mwalimu Nyerere aliposema:

> "Kukubali kufanywa vikaragosi vya viongozi ni dalili ya woga si dalili ya heshima ………kujenga mazoea ya kutii viongozi hata katika mambo haramu ni dalili ya woga ni kukaribisha udikteta".

Rais Mwinyi anamalizia kuwa Mwalimu aliandika kitabu kile kwa lugha kali na ghadhabu kubwa. Sasa anasema mfikirie yeye aliyekaa naye faragha na akayapokea hayo kwa ukali na ghadhabu ile ana kwa ana.

Nne, moja ya hoja zilizozaa kundi la G 55 ilikua suala Zanzibar kujiunga na Jumuiya ya Ushirikiano wa Nchi za kislam (Organization of Islamic conference). Rais Mwinyi anarudia kusema kuwa sababu ya kujiunga haikuwa mambo ya dini bali umaskini tu na matarajio ya misaada. Tatizo lilikuja pale ambapo baada ya mwanasheria mkuu wa serikali Mh. Damian Lubuva kushauri kuwa haikuwa sahihi kwa Zanzibar kujiunga pekee, Zanzibar iliomba uanachama kwa siri, na kuongopa kuwa serikali ya muungano iliridhia ombi hilo.

Tano, Rais Mwinyi anakiri kuwa Miongoni mwa mambo aliyomsumbua na kumsikitisha sana kipindi cha uongozi wake ni ugomvi na kufarakana ndani ya dini na madhehebu za dini, sambamba na tuhuma na mivutano baina ya dini moja na nyingine.

Kwa upande wa Wakristo ilitokea migogoro katika kanisa la Moravian huko Mbeya na Tabora. Mennonite na Assemblies of God huko Musoma, KKKT kwenye Dayosisi ya Mlima Meru, na kanisa Katoliki kuliibuka mvutano kuhusu sakramenti.

Kwa Waislam kulikuwa na migogoro ya ndani kwa ndani ikiwemo kati ya msikiti na waumini, huko Shinyanga, Arusha na Kagera. Mjini Bukoba kukawa na ugomvi juu ya kilichoitwa “Ijumaa” na “Adhuhuri”. Kulikuwa na ugomvi baina ya taasisi za kidini kama vile BAKWATA na BALUKTA na Baraza

la Misikiti Tanzania, BAMITA. Kulikuwa na juhudi za kuharibu jina zuri la BAKWATA.

Rais Mwinyi anasema kilichomuudhi sana, tena sana, ni vile mambo haya ya dini yalivyojipenyeza kwenye siasa. Anasema ilianza pia tabia mbaya ya baadhi ya watu kutumia maneno ya kejeli na dhihaka dhidi ya dini nyingine na pia vitendo vya kihuni kwa kisingizio cha dini.

Huko Zanzibar kulianza kupigwa vita watalii na utalii. Dar es Salaam vijana kama hao walianza kuvunja au kuchoma moto mabucha yanayouza nyama ya nguruwe.

Ukaenezwa uongo eti kwa kuwa mimi ni Muislam basi serikali yangu inaunga mkono vitendo hivyo vya kihuni. Pia zilienezwa uongo eti nilipendelea Waislam wenzangu kwenye uteuzi wa nafasi mbalimbali.

Kuhusu nguruwe, nilisema yule ambaye hakwaziki kula nguruwe, rukhsa. Na ambaye kwake ni haramu asilazimishwe kula.

Mwezi March 1993, alianzisha Baraza la Ushauri kuhusu dini ili kujenga uelewano na kuzuia migogoro ya dini.

Rais Mwinyi anabaini kuwa dhana yake ya "rukhsa' pia iliwafikia wafanyakazi kwa kuruhusu vyama huru vya wafanyakazi. Lakini ndani ya miaka miwili ya kuanzishwa OTTO, waliunga mkono mgomo mkubwa wa walimu na baadae wakaitisha mgomo March 1-3.

Sita, Rais Mwinyi anakiri kuwa kwa ujumla alianza vizuri sana na wafanyakazi ila alikuja kumaliza vibaya sana nao. "Mojawapo ya mambo yaliniuma sana" anasema Rais ni mauwaji ya wafanyakazi wanne na kujeruhi

wa vibaya sana kwa wengine 16 wakati wa mgogoro juu ya maslahi huko Kilombero. Hatua mbali mbali zilichukuliwa na serikali baada ya mkasa huu.

Rais Mwinyi anasema kipindi chake cha pili 1990-1995 kiligubikwa na mivutano mikubwa zaidi na kutofahamiana baina ya serikali na vyama vya wafanyakazi. Anasema "Na wengine kwa kweli walinikera na kuniudhi sana, wakiwema walimu". Pamoja na juhudi za kufikia muafaka, waliitisha mgomo, naikalazimu kuwadhibiti angalau kwa mda.

OTTU nao waliitisha mgomo, eti kwa sababu sikutekeleza ahadi niliyokuwa nimeitoa kwenye sherehe za wafanyakazi Mei Mosi, 1993 ya kuongeza mishahara. Wafanyakazi walinishukuru kwa migomo baada ya kupanua mipaka ya uhuru wao.

Wakaninunia kiasi cha kukataa kunialika kwenye sherehe za wafanyakazi Mei Mosi zilizofuata. Mwaka 1995 wakamwalika Mwalimu huko Mbeya akawakubalia. Mwalimu alinisema sana mimi na serikali yangu, na CCM, kwa kuacha misingi ya Ujamaa na Azimio la Arusha, pamoja na kubinafsisha mashirika ya Umma.

Wafanyakazi walifurahi sana tulivyosemwa pale Mbeya.

Wanafunzi wa vyuo vikuu nao hawakuwa nyuma. Huko Sokoine wanafunzi waligoma kulala watatu kwenye chumba, wakafanya fujo kubwa, ikabidi kuwasimamisha masomo zaidi ya nusu ya wanafunzi. Hapo chuo kikuu cha Dar es Salaam ilibidi niwarudishe makwao wanafunzi Mei 12, 1990 mpaka Januari 1991. Hii ilifuatia kukataa kwao kuingia madarasani na kubandika makaratasi kwenye mbao za matangazo na maeneo mengine yakiwa na matusi ya kila aina dhidi yangu binafsi na serikali. Rais Mwinyi anasema "Kwa

kweli wanafunzi wale walinivunjia heshima kiasi ambacho nilishindwa kuvumilia”.

Saba na mwisho ya changamoto, Rais Mwinyi anasema “Mojawapo ya mambo yaliyomsikitisha sana wakati wa urais wangu ni kuibuka mjadala mkali kuhusu kilichoitwa “Uzawa” hasa kuanzia mwaka 1993. Ugomvi huu ulitokana na Imani kwa watanzania wa kiafrika kwamba wenzao hasa wafanyabiashara waliweka fedha zao nyingi nje ya nchi, wao na wanafamilia wao walikuwa na uraia wa nchi tofauti tofauti ili iwawie raisi kukimbilia huko, kila kulipokuwa na ugumu wengi wao walikimbilia nchi nyingine, na walijijengea kinga ya kukamatwa walipofanya uhalifu kwa kuwahonga viongozi wa kisiasa na serikali, ikiwemo kwenye baadhi ya vyombo vya ulinzi na usalama.

Yakawepo maneno mengi, chuki na uadui baina ya wafanya biashara wa kiafrika na wa kihindi. Kwa upande wa wafanya biashara wa kiafrika mhusika mkuu alikua Bw. Reginald Mengi ambaye alipokea barua za vitisho kwa maisha yake na mali zake na ilibidi apewe ulinzi. Mchochezi mkuu alikuwa Rev. Christopher Mtikila. Ilisikitisha sana ushindani mkali baina ya wafanya biashara na wivu wa kibiashara unapogeuka kuwa uadui kwa msingi wa ubaguzi wa rangi, dini au kabila. Rais Mwinyi anasema alifanya juhudi kubwa kukemea jambo hili na pia kuchukua hatua madhubuti za kulinda watu na mali zao.